

MEDIA BRIEFS FOR MoM 10 APRIL, 2019

UHURU

❖ Kibano zaidi chaja kwa wapigaji wa dhahabu

Serikali imetangaza kibano zaidi kwa wanaoendesha vitendo vya udanganyifu katika sekta ya madini na kuwataka waliofungiwa kampuni za kuchenjua dhahabu kutoa ushirikiano wa udanganyifu walioutenda na wasipofanya hivyo watafungiwa milele. Akizunguzmza na Uhuru jijini Dar es salaam, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Profesa Simon Msanjila alisema walibaini kampuni hizo baada ya wizara kufanya operesheni kwa lengo la kuondoa udanganyifu mkubwa katika madini ya dhahabu nchini. (UK. 1&3).

❖ JAMVI LA HABARI

❖ Ukosefu waadilifu wafanyakazi Tume ya Madini wamkera Profesa Kikula

Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Idris Kikula amekerwa na kukasirishwa na ukosefu wa uadilifu kwa wafanyakazi wa Tume ya Madini katika baadhi ya Ofisi na kueleza kuwa, suala hilo halitavumilika kwa wanaokwenda kinyume na maadili ya kazi. Akizungumza na wafanyakazi wa Tume ya Madini Mkoa wa Morogoro katika siku ya kwanza ya ziara yake aliyoianza, Profesa Kikula amewaeleza wafanyakazi wa ofisi hiyo kuwa, yeye na viongozi wenzake wa tume wamekerwa na kusononeshwa na vitendo vya ukosefu wa uadilifu vinavyofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa Tume ya Madini. (Uk.3)

❖ Profesa Idris Kikula: Watumishi wa Tume ya Madini Morogoro fanyeni kazi kwa uadilifu

Mwenyekiti wa Tume ya Madini Prof. Idris Kikula na Dkt. Athanas Macheyeke wako mkoani Morogoro kwa ziara ya kikazi yya kukagua utekelezaji wa shughuli za Tume ya Madini katika Wilaya mbalimbali zinazofanya shughuli za madini sambamba na kutatua kero za wachimbaji na wadau mbalimbali. (Uk.14).

FAHARI YETU

❖ Wanaowazungusha Wawekezaji- JPM

Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Magufuli amewataka wawekezaji wote wanaotaka kuwekeza nchini wawekeze na kama kutakuwa na figisu ndani ya siku 30 wampatie taarifa. Rais alisema kumekuwa na kukwamishana kusiko kuwa kwa msingi kwasababu ya wivu wa kimaendeleo ambao hauna msingi. “Mimi ndiyo Rais kwa hiyo anayetaka kuwekeza katika viwanda au kitu chochote awekeze maana kuna wivu wa ajabu, laiti wazee hawa akina Katibu Mkuu Kiongozi wa zamani, Luhanjo na Spika wa Bunge wa zamani Anna Makinda wasinge wakaribisha wawekezaji hawa ingekuaje,” alisema. (Uk.2).

HABARI LEO

❖ Watendaji wanaozungusha wawekezaji kitanzini (Uk.1 &2)

MTANZANIA

❖ Profesa Kikula usisilalmike, chukua hatua.. (Tahariri)

..... Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Idris Kikula amesema amesikitishwa na tatizo la uadilifu na wafanyakazi wa tume hiyo kutokana na kushindwa kufuata maadili ya kazi. Profesa Kikula amesema hali hiyo inamfanya sasa asiwavumilie wale wote ambao wamekuwa vinara wa kurudisha nyuma maendeleo na juhudi zinazochukuliwa kila kukicha kupambana na wale wote wanaokwenda kinyume cha maadili.... Sisi MTANZANIA tunakukumbusha kuwa Profesa Kikula umefika wakati sasa wa kuchukua hatua, badala ya kubaki unanungu'nika kila wakati. Tunasema hiyo kwa sababu umepewa mamlaka kamili ya kuhakikisha eneo hilo linaondokana kwenye kashfa za aina hii.....(Uk.6).

MAJIRA

❖ Serikali yanunua mtambo wa madini

Serikali imenunua mtambo wa madini ambao utasaidia kufanya utafiti wa madini, sambamba na kuwasaidia wachimbaji wadogo katika shughuli za madini nchini. Akizungumza bungeni jana jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Madini Stanslaus Nyongo alisema kuwa, serikali imefikia

uamuzi huo kwa lengo la kuunga mkono wachimbaji wadogo nchini kote wakiwemo wachimbaji wa Kijiji cha Busiri Wilaya ya Biharamulo. (Uk.3)

❖ **Kikula akerwa na wafanyakazi kukosa uadilifu (Uk.9)**